# HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA

**ZIMANIMOTO SEKONDARI**
S.L.P 270
SONGEA
20/12/2020

**MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI**……………………………………………………………………………………

**MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI ZIMANIMOTO KIDATO CHA KWANZA 2021**

Nafurahi kukuarifu kuwa mwanao mtajwa hapo juu amechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza shule hii ya sekondari zimanimoto.

Shule hii ipo Mashariki mwa Manispaa ya songea, Umbali wa kilometa 5 kutoka Makao makuu ya Manispaa ya Songea.
Masomo kwa muhula wa kwanza mwaka 2020 yataanza tarehe **11/01/2021.**

Mwanao /Mwanafunzi anatakiwa kuletwa shuleni na Mzazi **saa 1:15 asubuhi** ya tarehe hiyo bila kukosa. Wanafunzi Watakaochelewa kuripoti tarehe tajwa nafasi yao itachukuliwa na wanafunzi wengine walio kwenye orodha ya akiba.

## MAAGIZO MUHIMU

### A . SARE YA SHULE

**WAVULANA**

[i] Mashati mawili [2] meupe mikono mifupi
[ii] Suruali mbili [2] za heshima [rangi ya kitambaa ni UGORO]
[iii] Mkanda wa suruali wenye upana wa inchi moja
[iv] Viatu vya ngozi vyeusi vyenye visigino vifupi jozi 2
[v] Sweta moja rangi ya suruali ya shule
[vi] Soksi nyeusi pea mbili
[vii] Mwavuli kwaajili ya kipindi cha mvua

**WASICHANA**

[i] Mashati meupe mawili mikono mifupi
[ii] Sketi mbili [2] zisizopungua linda kumi [rangi ya kitambaa ni UGORO]
[iii] Soksi nyeupe ndefu pea 2
[iv] Viatu vya ngozi vyeusi vya kufunika miguu, visigino vifupi.
[v] Sweta 1 rangi ya sketi ya shule
[vi] Mwavuli kwaajili ya kipindi cha mvua.

**NB;**

Mzazi upo **huru kununua Sare** za Mwanao kwenye duka lolote lenye Vitambaa vya Sare za shule unalolifahamu.

**Kwa msaada zaidi** mzazi unaweza kupata kitambaa cha **SURUALI, SKETI** pamoja na **Sweta** lenye rangi ya **UGORO** original inayohitajika shuleni kwenye duka la MWARABU **ABDU FASHENI.** Duka lake ni la nne ukitokea chini majimaji kupandisha kwenda juu katika mtaa wa uhindini ambapo kwa nje kuna kibao kilichoandikwa" **sare za shule Tanzania".** Suala la muhimu Ukifika kwenye duka hilo au lingine utakapo amua kununuasare za mwanao sisitiza kuwa upewe kitambaa rangi ya UGORO original **Kisichopauka Mapema**.

Ukichukua kitambaa rangi tofauti au kinachopauka au kuchuja Mapema mwanawe hatapokelewa na itakupasa ukaanze upya kumnunulia Sare tajwa inayohitajika hapa shuleni.

Hivyo mzazi unaombwa kufuata maelekezo vizuri kuepuka hasara.

Lengo kuu ni kufanana kwa sare zote kwa wanafunzi wote na kuwezesha hali ya vitambaa kutopauka Mapema kwa wanafunzi wetu wote na hivyo kuleta maana halisi ya neno Sare.

## [B] VIFAA VYA DARASANI

**Mzazi unatakiwa kumnunulia mwanao vifaa vya darasani vifuatavyo;**

-Penseli 2

-Peni 3 bluu 2 nyeusi

-Madaftari makubwa 9 aina ya kaunta quire two ($Q_2$)

-Daftari la summary 1 (Stiffcover).

-Madaftari saizi ya kati 08 aina ya superkid

-Mkebe mmoja (1) aina ya oxford au Marshal

-Rula ndefu moja

-Faili la Plastic 1 kwaajili ya kuhifahidhia pastpapers binafsi.

-Folder file 1 lenye kamba kwaajili ya kuhifadhia personal particulars

-Kichongeo 1 cha Penseli.

-Rimu moja A4 kwaajili ya Matumizi binafsi ya Mwanao katika Mazoezi na Majaribio mbalimbali kwa muhula mmoja unaoanza Januari hadi Juni 2021 au Ukiona inafaa unaweza Kumnunulia Rimu mbili ili atumie kwa Mwaka mzima Januari hadi Desemba 2021

-Mkoba mzuri wa kubebea daftari wenye hadhi (Mifuko ya vifungishio haikubaliki)

*Mzazi unajulishwa kumwandalia mwanao **Passport size 4** kwaajili ya Faili lake la usajili na photofolio ya wanafunzi kwenye ofisi ya Makamu , Taaluma na Malezi.

## [c] SARE ZA MICHEZO

Mzazi unatakiwa kumnunulia mwanao sare za michezo ambazo atatumia yeye mwenyewe wakati wa michezo kama ifuatavyo;

-Bukta 1 na T- shirt 1 zote rangi ya bluu.
-Trakisuti jozi 1 rangi ya bluu.
-Viatu vya michezo vya njumu kwa wavulana na raba za michezo kwa wasichana.
-Soksi ndefu { stocking} rangi ya bluu kwa Wavulana.

**NB:**

**{i} Mzazi unatakiwa kumleta mwanao shuleni tarehe iliyopangwa bila kukosa ili uweze kujaza na kusaini nyaraka muhimu za usajili shuleni. Mwanafunzi atakayekuja kuripoti bila Mzazi au Mlezi anayemsomesha au Kumlea hatapokelewa.**

**{ii} Mwanafunzi aje na sare zote za shule, vifaa vyote vya darasani,Mwavuli na sare za michezo kama ilivyoagizwa ili kukaguliwa na jopo la Walimu na Uongozi wa shule kwa lengo la kuthibitisha kuwepo kwa mahitaji hayo muhimu kwa kila mwanafunzi. Baada ya ukaguzi mwanafunzi atarudi na vifaa vyake vyote kwenda kutunza mwenyewe na kuja navyo shuleni pale inapohitajika kadri ya mpango na Ratiba ya shule.**

**{iii} Kila mwanafunzi anapaswa kuleta cheti cha kuzaliwa{original} na nakala 1 {copy yake }.**

# <u>SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE</u>

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na 25 ya mwaka 1978 aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya elimu nchini.

Mwanafunzi anatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo;

{i} Kuwa na Nidhamu nzuri na Heshima kwa viongozi , wafanyakazi wote, wazazi, Wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

{ii} Mahudhurio mazuri katika shughuli zote ndani na nje ya shule ni lazima .

{iii} Kutimiza kwa makini maandalio binafsi {self preparation in study}.

{iv} Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

{v} Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kuwepo ndani ya mipaka ya shule wakati wote unapoitajika kufanya hivyo kipindi chote cha masomo.

{vi} **Kutunza** usafi binafsi wa mwili,Mavazi,pamoja na mazingira ya shule.

{vii} Kuvaa sare za shule wakati wote mwanafunzi awapo shuleni au awapo nje ya shule katika safari za kishule.

{viii} Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa

<u>MAKOSA YAFUATAYO YANASABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE MARA MOJA.</u>

{i} Wizi

{ii} Uasherati

{iii} Ubakaji

{iv} Kugoma, kuchochea, kuongoza Migomo au kuvuruga amani na usalama wa shule.

{v} **Kupata mimba, kuharibu mimba (kutoa mimba) au kusababisha mimba** ndani na nje ya shule.

{vi} Kuharibu kwa makusudi mali za shule

{vii} Kudharau Bendera ya Taifa

{viii} Mwanafunzi kumiliki au kukutwa akiwa na simu ya mkononi .

{ix} Kupigana au kumpiga Mwanafunzi mwenziwe au raia mwingine.

{x} Kukataa adhabu halali kwa makosa/kosa halali.

{xi} Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine,mirungi,kubeli,n.k

**KARIBU ZIMANIMOTO SEKONDARI UNUFAIKE KWA ELIMU BORA**

...............................

**KOWERO KBY**

**MKUU WA SHULE**

HEADMASTER
ZIMANIMOTO S CONDARY SCHOOL
SONGEA-MUNICIPAL